JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU
## KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

www.kazi.go.tz

Toleo la 10 | Januari, 2023




Ijue
# SIKU YA BRELI DUNIANI
**04 JANUARI**



# Fahamu kuhusu Siku ya Nukta Nundu

Siku ya nukta nundu duniani huadhimishwa kila Januari 4 baada ya kupitishwa kwa azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Disemba 2018.

Tarehe hiyo inalingana na kuzaliwa kwa Louis Braille, ambaye akiwa na umri wa miaka 15, alizindua mfumo wa kusoma na kuandika wa nukta nundu kwa ajili ya matumizi na Watu wenye Ulemavu wa kutoona au uoni hafifu.

Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, ndio yenye jukumu la kuhakikisha masuala ya Watu wenye Ulemavu yanazingatiwa na kuhamasisha wadau kuendelea kusaidia mashine za nukta nundu ili kundi hilo liweze kufikia ndoto zao kielimu.

Mmoja wa wanafunzi ambaye anasoma shahada ya awali ya ualimu katika Chuo Kikuu Kishiriki cha DUCE, Agness Batega anazungumzia namna mfumo wa nukta nundu unavyomsaidia katika kufikia ndoto zake kielimu.

Alisema Watu wenye Ulemavu wanauwezo wa kufanya kazi kama watu wengine bila kikwazo chochote.

Naye, Katibu Mkuu wa Chama cha Wasioona, Udageja Manonga, alishauri jamii kutambua umuhimu wa mfumo huo ili kuandaa machapisho mbalimbali.




# Je Wajua?

Nukta nundu ni muwasilisho wa herufi kwa njia inayoshikika au kutambulika kwa video ambapo herufi na namba au hata noti za muziki na alama za kisanyansi zinachorwa kiasi kwamba mtu asiyeona au mwenye uoni hafifu anaweza kutambua na kusoma kama kawaida.

Matumizi ya nukta nundu huwezesha kundi hilo kusoma vitambu na majarida na hivyo kuimarisha ubobezi wao, uhuru na usawa katika nyanja mbalimbali.

Nchini Tanzania matumizi ya maandishi ya nukta nundu ni jambo la kawaida kwenye taasisi za elimu ikiwemo shule maalum kwa wasiioona na hata shule jumuishi.

"

Naishukuru serikali ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha kupata komputa hizi za nukta nundu zinatusaidia darasani kujifunza vizuri.

**Agness Batega**
*Mwanafunzi Chuo Kikuu Kishiriki cha DUCE*




# Waziri Ndalichako
# Atoa Somo kwa Vyama vya Wafanyakazi

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye ulemavu, Prof.Joyce Ndalichako amevitaka vyama vya wafanyakazi nchini kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia katiba, tararibu na miongozo waliyojiwekea.

Prof. Ndalichako alisema hayo Disemba 15, mwaka 2022 kwenye mkutano mkuu wa Chama Cha Walimu (CWT), uliofanyika jijini Dodoma.

Alisema ni muhimu vyama hivyo kuepusha migogoro mahala pa kazi huku akiwasihi waajiri kuvitambua na kuviheshimu vyama vya wafanyakazi.

“Baadhi ya waajiri wamekuwa ni kikwazo katika vyama vya wafanyakazi kufanya kazi zao naomba watambue vyama vya wafanyakazi vipo kwa mujibu wa sheria na ni daraja kati ya waajiri, serikali na wafanyakazi, kwa hiyo wawape nafasi wafanye kazi zao, waruhusu mabaraza ya wafanyakazi yafanyike kwa mujibu wa taratibu,”alisema.

Alibainisha kuwa milango ya serikali ipo wazi wakati wote kuhakikisha inazifanyia kazi changamoto za wafanyakazi kwa wakati ili kuwa na tija mahala pa kazi.

---

“Vyama vya Wafanyakazi ni kiungo mathubuti kati ya wafanyakazi na waajiri mahala pa kazi, hivyo vikitekeleza majukumu yao kwa weledi na kadri ya miongozo iliyojiwekea kwenye katiba na kanuni za kuendesha vyama daima kutakuwa na mahusiano mema mahala pa kazi,”

**Mhe. Prof. Joyce Ndalichako**
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu*

---



# Wakufunzi Stadi za Maisha Wahimizwa Kutoa Elimu kwa Vijana

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Patrobas Katambi amewataka wawezeshaji stadi za maisha kuhakikisha elimu hiyo inawafikia vijana wasio na Ulemavu na wenye Ulemavu ili waweze kutambua uwezo wao wa kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za ujenzi wa Taifa.

Naibu Waziri Katambi ametoa agizo hilo Disemba 17, 2022 wakati akifunga mafunzo ya stadi za maisha (Life Skills) kwa wakufunzi na watendaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu mkoani Mwanza huku akieleza lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha kuwa elimu ya stadi za maisha inajumuishwa kwenye afua na programu za kushughulikia changamoto za vijana ikiwemo vijana wenye Ulemavu.

Amesema kuwa, elimu ya stadi za maisha ni muhimu kwa kuwa inawajenga vijana na kuwapatia mbinu na maarifa ambayo yatawasaidia kutambua fursa zilizopo, namna ya kuweza kuzifikia na kujikwamua kiuchumi.

Ameongeza kuwa, ifikapo mwaka 2023 idadi ya waelimishaji wa stadi za maisha kitaifa inatarajiwa kufika 352 kutoka idadi ya wawezeshaji 142 waliopo kwa takwimu za mwaka 2022, ongezeko hilo itakuwa sawa na 60.2% ya lengo lililokusudiwa, hivyo kutakuwa na ongezeko kubwa la idadi ya waelimishaji rika wanaotarajiwa kutoa elimu ya stadi za Maisha kwa vijana wengi zaidi.

Aidha, Naibu Waziri katambi amesema kuwa pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kushughulikia masuala mbalimbali ya Watu wenye Ulemavu, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imeendelea kusimamia na kutekeleza maagizo yanayotolewa na viongozi mbalimbali ikiwemo Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu katika kuimarisha ustawi wa Watu wenye Ulemavu nchini, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya stadi za maisha kwa vijana wenye Ulemavu ili waweze kujitambua, kuwa na uthubutu, kufanya maamuzi sahihi na kuepuka vishawishi pamoja na mazingira hatarishi.

KATIBU MKUU
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**
Mji wa Serikali, **Mtumba**
Mtaa wa Kazi S.L.P 2890
40411 **DODOMA, Tanzania**
Barua pepe: *ps@kazi.go.tz*
**www.kazi.go.tz**

Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini